# Tutasonga Mbele, Hata Kama Tutalazimika Kutembea Katika Maji ya Mafuriko ya Pakistani: Jarida Nambari Thelasini na Sita (2022)



Ali Imam (Pakistan), *Untitled (Deserted Town with a Black Sun)*, 1956.

Marafiki Wapendwa,

Salamu kutoka dawati la Tricontinental: Institute for Social Research.

Majanga si kitu kigeni kwa watu Pakistani ambao wamekuwa wakikabiliana dhidi ya matetemeko ya ardhi makubwa, yakiwamo yale ya mwaka 2005, 2013, na 2015 (kwa kutaja yaliyoleta uharibifu mkubwa), pamoja na mafuriko kutisha ya mwaka 2010. Hata hivyo hakuna chochote ambacho kingeweza kuiandaa nchi ile inayoshika nafasi ya tano kwa idadi kubwa ya watu katika ulimwengu, dhidi ya matukio angamivu yaliotokea katika majira ya kipupwe cha mwaka huu, yaliyoanza kwa kupanda kwa jotoridi na vurumai za kisiasa kisha kufuatiwa na mafuriko yasiyomithilika.

Kuichokwa  serikali ya Pakistan kunafafanua hali ya hisia za umma. Taimur Rahman, katibu mkuu wa chama cha Mazdoor Kisan (‘Chama Cha Wakulima na Wafanyakazi ‘), alikiambia chanzo cha habari cha *Peoples Dispatch* kwamba baada ya mafuriko ya 2010, kulikuwa na ‘hali ya kubwa ya umma kukasirishwa, kulikotokana na jinsi ambavyo serikali haikufanya lolote kuhakikisha kuwa kunapotokea mtiririko mkubwa wa maji mwingine, basi unaweza kudhibitiwa’. Ushahidi wa kuwa fedha za kupunguza madhara ya janga lile ziliibwa na wanasiasa wala rushwa, na matajiri wachache wa tabaka la juu ulianza kujidhihiri katika kipindi cha baada ya 2010; kumbukumbu hizo zimeendelea kuwa hai. Watu wanaelewa sasa kuwa wakati vyombo vya kushughulikia majanga(disaster industrial complex) vinapotanuka, magenge ya rushwa nayo hushika kasi.

Tricontinental: Institute for Social Research imefanya kazi na  International People’s Assembly na kuandaa ;Red Alert no. 15,  hapa chini, katika mafuriko nchini Pakistan na madhara ya kisiasa ya janga hilo.



# Pakistan Chini ya Maji: Red Alert no. 15

## Je, mafuriko haya yanatokana na matendo Mungu?

Theluthi ya eneo la ardhi ya Pakistan ilikuwa kwenye mafuriko katika wiki ya mwisho ya mwezi Agosti. Taswira za Satelaiti zilionesha kusambaa haraka kwa maji ambayo yalivunja kingo za mto Indus, unaopita sehemu kubwa ya majimbo mawili ya , Balochistan, and Sindh. Mnamo Agosti 30, 2022, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa António Guterres aliita hali ile *'monsoon on steroids'*, ambapo maji ya mvua yaliwafagilia mbali na kuua zaidi ya watu 1,000 huku wengine milioni 33 wakiyakimbia makaazi yao. Hali ni tete, huku wale walioyakimbia makaazi yao wakiwa wakiwa katika hatari za dharura na za muda mrefu.

Watu walioweka kambi katika maeneo ya miinuko, kama vile katika barabara kubwa, wapo katika hatari ya kufa kwa njaa na kuambukizwa magonjwa yatokanayo na matumizi ya maji yasiyo salama kama vile kipindupindu, kuhara damu, kuhara na hepatitis. Katika masafa marefu, watu waliopoteza mazao-wima (miwa na pamba) na mifugo wana uhakika wa kufukarika. Waziri wa mipango wa Pakistan Ahsan Iqbal anakadiria kuwa uharibifu uliojitokeza utagharimu takribani Dola bilioni 10 .

Ukitazama kwa awali, sababu ya msingi ya mafuriko inaonekana kuwa mvua za ziada kubwa zilizofuata baada ya mvua za vuli zilizokuwa ambazo zimekwishavunja rekodi tayari.

Kipupwe chenye jotoridi lililofikia zaidi ya nyuzi 40°C kwa vipindi virefu kati ya Aprili na Mei kuliifanya Pakistan kuwa 'eneo lenye joto zaidi ulimwenguni ', kwa kadiri ya Malik Amin Aslam, waziri wa zamani wa mabadiliko ya tabia nchi. Miezi hiyo yenye joto kali imepelekea kuyeyuka kusikiko kwa kawaida kwa barafu katika eneo la kaskazini la nchi, ambapo maji yake yalikutana na maji ya mvua ya mafuriko yakichochewa na *'triple dip'* – kwa miaka mitatu mfululizo ya *La Niña cooling* (kupoa kwa muda mrefu kwa jotoridi katika uvungu wa bahari katika eneo la kati na mashariki ya bahari ya Pacific, kunakoambatana na mabadiliko katika tropiki ambayo ni upepo, mgandamizo na mvua. *Nina cooling ni kinyme cha El Nino*) katika eneo la bahari ya Pacific.

Kwa ziada, mabadiliko ya tabia nchi – yanayochagizwa kwa kiasi kikubwa na ubepari unaoendeshwa na nishati-ukaa katika ulimwengu – ndiyo yamesababisha pia kuyeyuka kwa barafu na na mvua kubwa pia.

Lakini kwa namna ya mafuriko yenyewe yalivyokuwa hayakutokana na muundo hali ya hewa yenye mtikisiko pekee. Kwa kiasi kikubwa madhara ya kuongezeka kwa maji kwa raia wa Pakistan yametokana kuharibiwa kwa misitu na ubovu wa miundo mbinu kama vile mabwawa, mifereji, na mikondo mingine ya maji kusikodhibitiwa. Mwaka 2019, Benki ya Dunia, walisema kwamba Pakistan ilikuwa ikakabiliwa na 'dharura ya kijani' kwasababu kila mwaka hekta 27,000 za misitu ya asili zinakatwa, hali inayopelekea ufyonzaji wa maji ya mvua katika udongo kuwa mgumu zaidi.

Zaidi, ukosefu wa uwekezaji wa serikali katika mabwawa na mifereji (ambayo Sasa yamechafuliwa na kujaa tope) kumepelekea ugumu zaidi katika kudhibiti viwango vikubwa vya maji. Kati ya mabwawa, mifereji na hifadhi za maji muhimu ni ni Sukkur Barrage, mfumo mkubwa wa kilimo cha umwagiliaji duniani wa aina yake, ambao unaunganisha mto Indus mto Sindh kwa eneo la kusini na hifadhi ya maji ya Mangla and Tarbela, ambao unachepusha maji kutoka mji mkuu wa Pakistan Islamabad. Ujenzi wa majengo unaofanywa na kampuni za ujenzi katika uwanda wenye kupitisha mafuriko unaongeza zaidi uwezo wa kutokea majanga ya kibinadamu.

Mungu anahusika kwa uchache sana na mafuriko haya. Asili imezuliwa janga la tabia nchi linalosababishwa na ubepari na kupuuzwa kwa usimamizi wa maji, ardhi, na misitu katika Pakistan.



Naiza H. Khan (Pakistan), *Graveyard at 11:23 am*, 2010

## Je, majanga yepi ya dharura yaitesayo Pakistan?

Maji ya mafuriko yamebainisha seti ya matatizo ya kudumu yanayoilemaza Pakistan. Utafiti wa mwezi Mei, kabla ya mafuriko, ulionesha kuwa 54% ya watu wanaona kuwa mfumuko wa bei ndilo tatizo la msingi kwao. Mpaka kufikia Agosti, kitengo cha takwimu cha Pakistan kiliripoti kuwa kigezo cha manunuzi ya jumla, ambacho kinapima wastani wa mfumuko wa bei za bidhaa, kiliongezeka kwa 41.2% wakati kasi ya ukuaji mfumuko wa bei kwa mwaka ulikuwa 27%. Licha ya kuwa mfumuko wa bei unatokea ulimwenguni kote na utambuzi kwamba gharama zitakazotokana na mafuriko haya zinatakuwa dola bilioni 10, Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) limeahidi dola bilioni 1.1 zikiwa zimeambatana na masharti makali lukuki kama vile 'prudent monetary policy'. Ni jinai kwa IMF kulazimisha masharti makali mno ilhali miundombinu ya Kilimo ya nchi ile imeharibiwa kabisa (kitendo hiki kinakumbusha sera ya kikoloni ya Uingereza ya kuhakikisha uendelezwaji wa usafirishwaji nje wa zao la ngano toka India katika kipindi cha ukame mkali wa Bengal mwaka 1943). Vigezo vya njaa vya Ulimwengu tayari vinaiweka Pakistan katika nafasi ya 92 kati ya nchi 116 kutokana na tatizo lake la njaa –kabla ya mafuriko – katika kiwango cha juu. Hata Sasa, kama ambavyo hakuna miongoni mwa vyama vya siasa vya kibwanyenye kilichoyachukulia matokeo haya ya kitafiti kwa uzito, bila shaka, hali mbaya ya kiuchumi itaongezeka huku kukiwa na kuimarika kudogo.

Hili linatupeleka mpaka katika mgogoro mkubwa wa kisiasa. Tangu kupata uhuru wake kutoka kwa Uingereza mwaka 1947, miaka 75 iliyopita, Pakistan imekuwa na mawaziri wakuu 31. Mwaka 2022 mwezi Aprili , Waziri Mkuu wa thelasini, Imran Khan aliondolewa na kuwekwa Waziri Mkuu wa sasa Shehbaz Sharif. Khan, ambaye anakabiliwa na mashitaka ya ugaidi na dharau kwa mahakama, , yadaiwa kuwa serikali yake iliondolewa kwa usaidizi wa Washington (Marekani) kwa kuwa ilikuwa na ukaribu wa kimashirikiano na Urusi. chama cha Khan cha Pakistan Tehreek-e-Insaf (PTI ama 'Chama Cha Haki') ambacho hakikushinda viti vingi bungeni katika uchaguzi wa mwaka 2018, ambao uliiacha serikali yake ya umoja katika hali ngumu ikitegemea wabunge wachache kuinusuru. Hilo ndilo lililofanywa na upinzani, ambao uliyatwaa madaraka kwa kutumia janja-janja za bunge, bila kutafuta uhalali mwingine toka kwa umma. Tangu kuondolewa kwake, umashuhuri wa Imran Khan na PTI umepanda katika Pakistan, huku kikishinda viti 15 kati ya 20 katika uchaguzi mdogo wa Julai huko Karachi na Punjab, kabla ya janga la mafuriko. Sasa , kwa kadiri ya hasira dhidi ya serikali ya Sharif inavyozodi kupanda kwasababu ya kasi yake ndogo ya kusaidia wahanga wa mafuriko, mgogoro wa kisiasa utazidi kukua.



Huma Mulji (Pakistan), *Tip Top Dry Cleaners*, 2015.


## Majukumu gani yaliyopo mkononi?

Pakistan inateswa na ‘ubsguzi katika tabia nchi (climate apartheid)’. Nchi hii ina watu takribani Milioni 230 inachagiaa 1% pekee katika kuzalisha hewa chafu ulimwenguni, lakini inatishiwa na vilivyo na hatari kubwa ya nane ya tabia nchi ulimwenguni. Kushindwa kwa nchi za kibepari za Magharibi kutambua uharibifu wao kwa tabia ya nchi ya sayari hii kunamaanisha kuwa nchi kama Pakistan, ambazo zina kiwango kidogo cha uzalishaji hewa chafu, tayari zinapitia kwa kiwango kikubwa kibaya cha mabadiliko ya tabia ya nchi kwa kasi. Nchi za kibepari za magharibi lazima zitoe usaidizi wa kutosha katika Agenda ya Kimataifa ya Mapambano ya Tabia Nchi.

Kani za mrengo wa kushoto na mrengo wa kimeendelea – mfano Chama Cha Mazdoor Kisan waliratibu kampeni ya kuchangisha michango ya hali na mali kukabiliana na mafuriko katika majimbo manne ya Pakistan.

Wanawafikia watu na wakiwa na mahitaji ya chakula ili kutatua hatari ya lufa kwa katika maeneo yasiyo rahisi kufikika, hususani maeneo ya vijijini. Watu wa mrengo wa kushoto nchini Pakistani

wanashinikiza serikali kugeuza wimbi la ukali wa mfumuko wa bei ambao bila shaka unazidisha janga la kibinadamu.




Katika majira ya kipupwe cha mwaka 1970, mafuriko ya kasi katika uwanda wa milimani wa Balochistan yalisababisha uharibifu mkubwa. Miezi michache baadaye katika uchaguzi mkuu

mshairi Gul Khan Nasir wa chama cha National Awami alishinda kiti katika bunge la jimbo la Balochistan na kuwa waziri wa elimu, afya habari, ustawi wa jamii na utalii. Gul Khan Nasir alitumia msukumo wake wa umarx kufanya kazi ya kujenga uwezo wa jamii ya watu Baloch (ikiwamo kushughulikia uanzishwaji wa shule/ chuo pekee cha afya huko Quetta, mji mkuu wa jimbo la Balochistan). Aliondolewa ofisini kwa njia zisizokuwa za kidemokrasia, Nasir alirudishwa gerezani, mahala ambapo tayari alikuwa amekwishapazoe toka miaka iliyopita. Akiwa gerezani, aliandika wimbo wake, 'Demaa Qadam' (' Songa Mbele') moja kati ya stanza zake, inaonekana kuweza kuelezea mguso ya nchi yake ya asili, miaka 50 baadaye:

> Ikiwa anga lililo juu ya vichwa vyenu
> limekasirika, na hasira kuu,,
> tufani na mvua na radio na upepo.
> Usiku umekuwa kiza mithili ya lami.
> Ardhi imekuwa kama moto.
> Nyakati zimekuwa katili.
> Lakini shabaha yenu imesalia kuwa ileile:
> Songeni, Songeni, Songeni Mbele.
> .

Kwa Huba,

Vijay

Jarida hili limetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na Muhemsi Mwakihwelo. muhemsimwakihwelo@gmail.com